**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)**

**SURA YA 287**

**SHERIA NDOGO**

(Imetungwa chini ya kifungu cha 153)

# SHERIA NDOGO YA (UDHIBITI UTORO NA UPATIKANAJI WA CHAKULA ELIMU YA MSINGI) YA HALMASHAURI YA WILAYA YA NYANG'HWALE YA MWAKA 2024.

MPANGILIO WA VIFUNGU

*Kifungu* *Jina*

**SEHEMU YA KWANZA**

**MASHARTI YA AWALI**

1. Jina fupi na mwanzo wa kutumika
2. Matumizi
3. Tafsiri

**SEHEMU YA PILI**

*(a) Wajibu wa mzazi*

4. Wajibu wa mzazi

*(b) Wajibu wa mwanafunzi*

5. Wajibu wa mwanafunzi

**SEHEMU YA TATU**

6. Wajibu wa mwalimu mkuu au mkuu wa shule
7. Ukaguzi wa elimu

**SEHEMU YA NNE**

8. Wajibu wa Afisa Mtendaji
9. Wajibu wa kamati au bodi ya shule

**SEHEMU YA TANO**

10. Makosa kwa mwalimu
11. Adhabu kwa ujumla

**SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)**

**SURA YA 287**

**SHERIA NDOGO**

(Imetungwa chini ya kifungu cha 153)

**SHERIA NDOGO YA (UDHIBITI UTORO NA UPATIKANAJI WA CHAKULA ELIMU YA MSINGI) YA HALMASHAURI YA WILAYA YA NYANG'HWALE YA MWAKA 2024.**

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina na mwanzo wa kutumika

1. Sheria Ndogo ya (Udhibiti Utoro na upatikanaji wa Chakula Elimu ya Msingi) ya Halmashauri ya wilaya ya Nyang'hwale ya mwaka 2024 na itaanza kutumika tarehe itakayotangazwa katika gazeti la serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale.

Tafsiri

3. Katika sheria hii:-

**"Afisa elimu"** ni mtumishi yoyote aliyekasimiwa jukumu la kusimamia elimu ya msingi katika Halmashauri ya wilaya ya Nyang'hwale.

**"Afisa mtendaji"** ni mtendaji wa kata au wa kijiji."

**"Elimu msingi"** maana yake ni Elimu ya awali mpaka kidato cha nne.

**"Halmashauri "** maana yake ni Halmashauri ya wilaya ya Nyang'hwale au Kijiji husika kulingana na muktadha wa suala husika.

**"Mkaguzi wa shule"** Ni mtumishi wa umma mwenye dhamana ya kukagua shule za Msingi na Sekondari.

**"Mtoro"** maana yake ni mwanafunzi ambaye hajahudhuria shule kuanzia siku moja au zaidi katika mwaka wa masomo bila sababu za msingi.

**"Mwalimu"** maana yake ni mtu mwenye taaluma ya ualimu anayefundisha katika shule za Msingi au Sekondari zilizopo katika Halmashauri ya wilaya ya Nyang'hwale.

**"Mwanafunzi"** ni mtoto aliyeandikishwa shule na ambaye hajamaliza elimu ya Msingi.

**"Mzazi"** maana yake ni baba, mama au mlezi wa mwanafunzi aliyeandikishwa shule mwenye dhamana ya kumtunza na kumlea mwanafunzi huyo.

**"Shule"** maana yake ni taasisi inayotoa elimu ya msingi katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale.

## SEHEMU YA PILI

## WAJIBU WA MZAZI NA MWANAFUNZI

*(a) Wajibu wa mzazi*

4. 1) Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii, kila mzazi atakuwa na wajibu ufuatao;
   a) atahakikisha mtoto mwenye umri kuanzia miaka mitano anaandikishwa na kuhudhuria shule kwa ajili ya elimu ya msingi hadi atakapohitimu;
   b) kuchangia chakula au fedha kwa ajili ya chakula cha mwanafunzi au michango mingine kwa kuzingatia makubaliano kati ya Kamati au Bodi ya shule na wazazi;
   c) kufuatilia mahudhurio na maendeleo ya mwanafunzi shuleni;
   d) kuhakikisha mwanafunzi ana vifaa na sare za shule;
   e) kuhudhuria vikao vya wazazi shuleni;
   f) kutoa taarifa kuhusu kikwazo au sababu yoyote itakayomfanya mwanafunzi kushindwa kuhudhuria shuleni;
   g) kutoa taarifa kwa afisa mtendaji, polisi au shuleni kuhusu vitendo vya ukiukwaji wa maadili au nidhamu ya mwanafunzi;
   h) kufuatilia afya ya mwanafunzi kipindi akiwa shuleni au nyumbani na;
   i) kuhakikisha mwanafunzi anakuwa na bima ya afya kwa kuzingatia sera ya nchi.

2) mzazi atakayekiuka wajibu huu atakuwa ametenda kosa kwa mujibu wa sheria ndogo hii.

*(b) Wajibu wa mwanafunzi*

5. 1) Mwanafunzi atakuwa na wajibu ufuatao:
    a) kuhakikisha anahudhuria shuleni siku zote za masomo;
    b) kuhakikisha anahudhuria vipindi vyote vya masomo vinavyomuhusu na;
    c) kuhakikisha anatii sheria za shule, za nchi na miongozo mbalimbali ya kielimu;
    d) kushiriki katika utamaduni, sanaa na michezo mbalimbali kwa mujibu wa miongozo ya nchi na;
    e) kutoa taarifa kwa walimu, mzazi, polisi, afisa mtendaji au kwa mtu yeyote ya vitendo vya ukiukwaji wa maadili vinayofanyika shuleni.

2) Mwanafunzi atakayekosa kuhudhuria shuleni kuanzia siku moja bila sababu ya msingi atakuwa amehesabiwa kuwa mtoro na atakuwa ametenda kosa na atawajibika kwa kuzingatia adhabu zilizotolewa katika Jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hii.

## SEHEMU YA TATU

## WAJIBU WA MWALIMU MKUU, MKUU WA SHULE NA UKAGUZI WA ELIMU

Wajibu wa mwalimu mkuu au mkuu wa shule

6. 1) Mwalimu mkuu au mkuu wa shule anapaswa kuandaa taarifa ya mahudhurio wanafunzi ya kila mwezi na kuiwasilisha kwa afisa mtendaji wa Kijiji, Kata na nakala iwasilishwe Halmashauri ya Wilaya kwa ajili ya ufuatiliaji wa wanafunzi watoro.

    2) Mwalimu mkuu au mkuu wa shule ana wajibu wa kuhakikisha wanafunzi walioko hosteli wanaishi katika mazingira safi, bora na salama.

Ukaguzi wa elimu

7. 1) Afisa Elimu au mkaguzi wa shule anaweza kufanya ukaguzi katika shule yoyote ambayo ipo chini yake na kuwasilisha taarifa ya utoro wa wanafunzi kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri.

2) Afisa Elimu ana wajibu wa kufanya ufuatiliaji na kuhakikisha kuwa wanafunzi watoro wanachukuliwa hatua stahiki.

3) Afisa Elimu ana wajibu wa kuhakikisha wanafunzi walioko hosteli wanaishi katika mazingira safi, bora na salama.

**SEHEMU YA NNE**

**WAJIBU WA AFISA MTENDAJI, KAMATI NA BODI YA SHULE**

Wajibu wa Afisa Mtendaji

8. 1) Afisa mtendaji wa kijiji ana wajibu wa kuwasilisha majina ya watoto wenye sifa za kuanza shule kwa mwalimu mkuu kabla ya kufunguliwa kwa muhula mpya wa masomo kwa mwaka husika.

2) Afisa mtendaji ana wajibu wa kuhakikisha watoto wote wenye umri wa kuanzia miaka mitano wanandikishwa kuanza elimu ya msingi.

3) Afisa Mtendaji wa Kijiji na Kata watahakikisha wanafunzia wote wanahudhuria shuleni bila kukosa.

4) Afisa Mtendaji wa Kijiji au Kata ana wajibu wa kufungua kesi mahakamani dhidi ya mzazi, mlezi, mtu yeyote au mwanafunzi atakayekiuka Sheria Ndogo hii au sheria nyingine za nchi. Na hii, haimzuii mtu mwingine kufungua kesi ya aina hiyo ikiwa afisa mtendaji hajafungua kesi mahakamani.

Wajibu wa kamati au bodi ya shule

9. Wajibu wa kamati au Bodi ya shule utakuwa kama ifuatavyo:-

1) Kuhakikisha kuwa wanafunzi wote walioandikishwa shuleni wanahudhuria hadi watakapomaliza Elimu ya Msingi.

2) Kuhakikisha kuwa walimu wote wanazingatia ratiba ya shule.

3) Kuhakikisha kuwa wanafunzi wanakula chakula shuleni.

4) Kuhakikisha wanafunzi walioko hosteli wanaishi katika mazingira safi na bora.

## SEHEMU YA TANO

## MAKOSA KWA MWALIMU NA ADHABU KWA UJUMLA

Makosa kwa mwalimu

10. Itakuwa kosa kwa mwalimu;

1) Kumtumikisha Mwanafunzi kazi yoyote ambayo haiko katika mpango wa kazi za shule ambayo haijaidhinishwa na kamati au bodi ya shule.
2) Kutoa adhabu zilizokatazwa chini ya Sheria yoyote, Kanuni, Amri na miongozo ya nchi.
3) Kumsimamisha kuhudhuria shule mwanafunzi kwa kosa ambalo kimsingi halikusababishwa na mwanafunzi bali mzazi wake au mtu mwingine.
4) Kumfanyia mwanafunzi vitendo ambavyo viko kinyume na maadili ya kazi ya ualimu.

Adhabu kwa ujumla

11. 1) Mtu yeyote atakayekuwa na mahusiano ya mapenzi na mwanafunzi atakuwa ametenda kosa, akipatikana na hatia adhabu itatolewa kwa mujibu wa Sheria za nchi.

3) Mwanafunzi akitenda kosa na kupatikana na hatia ataadhibiwa kwa mujibu wa Sheria za shule, Sheria Ndogo hii, Sheria ya Elimu Sura 353 pamoja na kanuni na miongozo yake, Sheria ya Mtoto, Sura 13 au Sheria nyingine yoyote inayohusika.
4) Mtu yeyote atakaye mtorosha mwanafunzi shule kwa lengo lolote atakua ametenda kosa.
5) Mzazi au mlezi atakayeshindwa kumuandikisha mtoto shule kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia kwa kosa la kwanza atahukumiwa kulipa faini isiyopungua shilingi elfu thelathini na isiyozidi elfu hamsini, na kwa kosa la pili faini isiyopungua shilingi elfu hamsini na isiyozidi laki moja au kifungo cha miezi sita au vyote kwa pamoja.
6) Mzazi au mlezi atakayesababisha mwanafunzi kushindwa kuhudhuria shuleni atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atalipa faini

isiyopungua shilingi elfu ehelathini na isiyozidi elfu hamsini au kifungo cha miezi sita au vyote kwa pamoja.

7) Mzazi au mlezi atakayekiuka makubaliano ya kikao cha wazazi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atalipa faini isiyopungua Shilingi elfu thelathini na isiyozidi elfu hamsini au kifungo cha miezi sita au vyote kwa pamoja.

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale imewekwa kwenye Sheria Ndogo hii kwa kufuatia azimio lililopitishwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale uliofanyika tarehe ............mwezi ..........Mwaka ........... na kushuhudiwa Nembo hiyo ikiwekwa mbele ya:-

...............................

HUSNA TONI

Mkurugenzi Mtendaji (W)

**Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale**

...............................

JOHN ISSACK JOHN

Mwenyekiti wa Halmashauri

**Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale**

NAKUBALI,

Dodoma.

MOHAMED OMARY MCHENGERWA (Mb)

TAREHE...........................

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.